


# Wimbo wa Sakima



✎ Ursula Nafula  
🔊 Peris Wachuka  
📄 Ursula Nafula  
😊 Kiswahili  
📖 Level 3

This story originates from the African Storybook ([africanstorybook.org](http://africanstorybook.org)) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.  
<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>



Sakima aliishi na wazazi wake na dada yake wa miaka minne. Waliishi katika shamba la mtu tajiri. Nyumba yao ya nyasi ilikuwa mwisho wa safu ya miti iliyopendeza.



Tajiri alifurahi sana kumwona mwana wake tena. Alimzawadia Sakima kwa kumliwaza. Aliwapeleka mwanawe na Sakima hospitali ili Sakima aweze kusaidiwa kuona tena.




Sakima alipokuwa na umri wa miaka mitatu, aliugua na kupoteza uwezo wa kuona. Hata hivyo, Sakima alikuwa mvulana mwenye kipaji.




Wakati huo huo, watu wawili walikuja wakiwa wamembeba mtu kwenye machela. Walimkuta mwana wa tajiri akiwa amechapwa na kuachwa kando ya barabara.



Sakima alitenda mambo mengi ambayo wavulana wengine wa umri wake hawakufanya. Kwa mfano, angeketi na watu wazima na kujadili mambo muhimu.



Sakima alipomaliza kuimba wimbo wake alianza kuondoka. Tajiri alitoka nje kwa haraka na kusema, "Tafadhali, imba tena."




Wafanyakazi waliacha kazi zao.  
Wakasikiliza wimbo mzuri wa Sakima. Hata  
hivyo, mwanamume mmoja alisema,  
“Hakuna aliyefaulu kumtuliza bwana. Je,  
huyu mvulana asiyeona anatikiri  
atamtuliza?”



Wazazi wa Sakima walifanya kazi katika  
nyumba ya yule tajiri. Walitoka nyumbani  
asubuhi na mapema na kurudi jioni.  
Sakima aliachwa na dada yake.




Sakima alipenda kuimba nyimbo. Siku moja mama yake alimuuliza, "Sakima, unajifunza nyimbo hizi kutoka wapi?"



Alisimama chini ya dirisha moja kubwa na kuanza kuimba wimbo wake alioupenda. Pole pole, kichwa cha tajiri kilionekana dirishani.



Siku iliyofuata, Sakima alimwomba mdogo wake amwongoze hadi kwenye nyumba ya tajiri.



Sakima alimjibu, "Nazisikia akilini mwangu kisha nazimba."



Sakima alipenda kumwimbia mdogo wake hasa akihisi njaa. Dada yake alimsikiliza na kucheza.




Hata hivyo, Sakima hakukata tamaa. Mdogo wake alimpa moyo. Alisema, "Nyimbo za Sakima hunituliza mimi nikiwa na njaa. Zitamtuliza tajiri vile vile."

“Labda atafurahi tena nikimwimbia,”  
 Sakima aliwaambia wazazi wake. Wazazi  
 wake walidharau wazo lake. “Yeje ni tajiri  
 sana. Wewe ni mvlana asiyeona.  
 Unadhani wimbo wako utamsaidia?”



“Naomba uimbe tena na tena, Sakima,”  
 mdogo wake alimsihi. Sakima alikubali na  
 kuimba mara nyingine.





Jioni moja, wazazi wake waliporudi nyumbani, walikuwa kimya sana. Sakima alijua kwamba lazima kulikuwa na jambo baya.



“Kuna shida gani, mama, baba?” Sakima aliuliza. Sakima aligundua kwamba mwana wa tajiri wao alikuwa amepotea. Tajiri alihuzunika na kuwa na upweke mkubwa.